# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

ISSN 1821 - 8253

TOLEO MAALUM



# Kilele cha maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar

- Hotuba ya Rais imebainisha mafanikio makubwa ndani ya kipindi cha mwaka 2015

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Said J.Ameir

**Waandishi**
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed

## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.

Jarida hili linatolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.Box: 2422
Zanzibar - Tanzania
Phone: +255 223 081/5
Fax: 024 223 3722
Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz

# Maoni ya Mhariri

## Sherehe za Mapinduzi ni kwa wanaojali utu wao, heshima yao na uhuru wa kujitawala.

Miaka 52 ni zaidi ya kipindi kinachotosha kupima na kufahamu mafanikio na mwelekeo wa maisha ya mwanadamu au hata taifa ambalo kwa muda mrefu lilitawaliwa na baadae kupata uhuru wa kujiamulia mambo yake.

Miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar inatosha kabisa kwa wananchi wa Zanzibar kujitathmini walikotoka, walipo na waendako. Historia inatufundisha kuwa kabla ya miaka 52 iliyopita Zanzibar ilikuwa chini ya utawala wa kisultani na ukoloni wa Kingereza ambao ulidumu kwa miaka 132.

Serikali hiyo ya kikoloni ilikoma tarehe 12 Januari 1964 baada ya wananchi wa Zanzibar chini ya kiongozi wao Jemedari wa Mapinduzi marehemu Mzee Abeid Karume kukataa vitendo vya kudharauliwa, kunyanyaswa, kubaguliwa na kutoheshimiwa kwenye ardhi yao.

Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964 ni mwanzo mzuri wa kupima maendeleo ya Zanzibar kwa kulinganisha tunakutoka kabla ya Mapinduzi, tulipo baada ya Mapinduzi na twendako ambako muelekeo wetu unaoneshwa kwenye Mipango mikuu ya kitaifa na kimataifa ikiwemo (MKUZA II), Dira 2020, Malengo ya Millennia na bila ya shaka Ilani za vyama vya siasa tunavyovichagua kutuongoza.

Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar ni ushahidi uliowazi kwamba mafanikio makubwa yamepatikana kwa wananchi wa Zanzibar ndani ya kipindi hiki cha miaka 52 ikilinganishwa na miaka 132 ya utawala wa kikoloni.

Licha ya wananchi wa Zanzibar kujivua na matatizo ya kudharauliwa,kunyanyaswa, kubaguliwa na kutoheshimiwa kwenye ardhi yao, wananchi wa Zanzibar mjini na mashamba wanayo fahari kubwa ya kujivunia matunda ya Mapinduzi kwa kupata huduma muhimu za kijamii bila ya malipo na bila ya kubaguliwa kwa njia yoyote.

Hatua hiyo inafuatia uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kutangaza elimu bure, matibabu bure na kuwapatia wananchi eka tatu tatu za ardhi kwa ajili ya kilimo mara tu baada ya Mapinduzi, mambo ambayo hayakuwa yakipatikana wakati wa utawala wa kikoloni.

Katika kipindi hiki cha miaka 52 ya Mapinduzi, kila mtu ameweza kushuhudia kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar katika kila sekta kila mwaka. Kwa mfano katika mwaka uliopita, licha ya kuendelea kuwepo kwa matukio mbali mbali yanayoathiri kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika.

Mwaka 2014 Pato halisi la Taifa lilikua na kufikia asilimia 7.0. Hali hii imechangiwa zaidi na kuimarika kwa sekta ya viwanda na sekta ya huduma kwa kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini kutokana na kuwepo kwa vivutio vya utalii na amani na utulivu. Kadhalika, Pato la Mtu binafsi nalo limeongezeka hadi kufikia TZS 1,552,000 (USD 939) mwaka 2014 ikilinganishwa na TZS 1,384,000 (USD 866) mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Sekta nyengine zote za kijamii kama vile afya, elimu na huduma za maji safi na salama nazo zimeimarika sana ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Kisiasa, nchi imepiga hatua kubwa kwa kuweza kupanua wigo wa demokrasia ambapo wananchi wapo huru kuchagua viongozi wao wanaowataka kupitia vyama tofauti vya siasa. Uamuzi wa kurejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa ulipitishwa rasmi mwaka 1992 kutokana na mabadiliko ya kisiasa duniani.

Kutokana na mafanikio hayo, kusherehekea Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964 kila mwaka ni jambo muhimu na la fahari kwa kila Mzanzibari mwenye kujali kuheshimiwa na kuthaminiwa utu na uhuru wake wa kujitawala.

**Mapinduzi Daima.**

# Yaliyomo


Kilele cha maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar **uk. 4**



Muziki wa taarab kielelezo cha Zanzibar **uk. 12**



Uwekaji wa Mawe ya Msingi wodi ya watoto pamoja na Kinamama Mnazi Mmoja **uk. 16**



Wanakijiji wa Mnarani Pemba wafurahia kupata skuli ya kisasa **uk. 18**



Dk. Shein aandika historia mpya Pemba **uk. 20**



Dk. Shein ametaka studio ya kurekodia muziki, filamu itumike kuinua vipaji vya sanaa **uk. 25**




# Kilele cha maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar

- Hotuba ya Rais imebainisha mafanikio makubwa ndani ya kipindi cha mwaka 2015



Tarehe 12 Januari ya kila mwaka kuanzia mwaka 1964 imekuwa ni siku adhimu na muhimu kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kutokana na kuikumbuka siku ambayo wananchi wa Zanzibar waliikata minyororo ya utawala wa kikoloni na kisultani ambao ulidumu kwa miaka 132.

Ni siku hii ambayo wananchi wanyonge wakioongozwa na Chama cha Afro Shirazi, walijitolea muhanga kufanya Mapinduzi dhidi ya wakoloni, mabwanyenye na mabepari waliokuwa wakiendeleza vitendo vya udhalilishaji, dhulma, unyonyaji na ubaguzi kwenye ardhi ya wananchi wa Zanzibar.

Kimsingi, madhila waliyotendewa wananchi wanyonge wa Zanzibar yalikita katika masuala yote muhimu katika maisha ya mwanadamu yakiwemo kubaguliwa katika elimu, matibabu, makaazi, matumizi ya ardhi na ubaguzi wa kukoseshwa haki za kiraia katika nchi yao wenyewe.

Mambo hayo yote leo yanabaki kuwa ni historia baada ya Waasisi wa Mapinduzi wakiongozwa na Jemedari wake Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Chama cha ASP kufanya Mapinduzi tarehe 12 Januari, 1964.

Mapinduzi hayo ndiyo yaliyohitimisha utawala wa kikoloni na kuanzisha historia mpya ya utawala wa wanyonge wa Zanzibar na kupata uhuru wao wa kweli, unaozingatia misingi ya usawa, utu na kurejesha heshima ya wafanyakazi na wakulima ambayo ilipotea kutokana na kutawaliwa.

Kwa miaka 52 sasa Wazanzibari wamepata fursa ya kujiamulia mambo yao wenyewe huku wakishuhudia maendeleo makubwa katika sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii licha ya ongezeko kubwa la idadi ya watu. Pamoja na uhuru huo, Zanzibar imepata mafanikio makubwa ndani ya miaka 52 ikilinganishwa na miaka 132 ya ukoloni. Mapinduzi ya Zanzibar yameleta faraja kwa wananchi wote wa Zanzibar bila ya kujali itikadi zao za kisiasa, dini, rangi, kabila wala uzawa.

Mafanikio ya Serikali katika kuleta maendeleo yamekuwa yakionekana kunawiri kadri siku zinavyoendelea na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo huonekana kila baada ya kipindi maalum.

Licha ya kuendelea kuwepo kwa matukio mbali mbali yanayoathiri kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika katika kila mwaka.

Katika hotuba yake kwa taifa kwenye kilele cha maadhimisho ya sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alibainisha maeneo kadhaa ambayo Serikali anayoiongoza imepata mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita pamoja na kuwepo baadhi ya changamoto.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikagua gwaride la Vikosi vya Ulinzi lililoandaliwa rasmi katika kilele cha sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan Studium Mjini Unguja tarehe 12 Januari, 2016,

Mwaka 2014 Pato halisi la Taifa lilikua na kufikia asilimia 7.0. Hali hii imechangiwa zaidi na kuimarika kwa sekta ya viwanda na sekta ya huduma kwa kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini kutokana na kuwepo kwa vivutio vya utalii na amani na utulivu. Kadhalika, Pato la Mtu binafsi limeongezeka hadi kufikia TZS 1,552,000 (USD 939) mwaka 2014 ikilinganishwa na TZS 1,384,000 (USD 866) mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, pato la mtu binafsi lilitakiwa lifikie TZS 884,000 ifikapo mwaka 2015. Ni dhahiri kwamba pato la mtu binafsi limepindukia kiwango kilichokadiriwa.

Katika mwaka 2015, kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini imeendelea kuwa ya tarakimu moja kutoka asilimia 5.6 mwaka 2014 kufikia asilimia 5.7 mwaka 2015. Serikali inaendelea na juhudi za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei nchini kwa kupunguza ushuru wa bidhaa muhimu zinazoingizwa nchini na kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia pembejeo kwa bei nafuu ili kuongeza uzalishaji wa mazao.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza ufanisi katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti uvujaji wa mapato hayo. Katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/2016, mapato ya ndani yalifikia TZS Bilioni 188.4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2014/2015 ambapo TZS Bilioni 172.5 zilikusanywa, sawa na ongezeko la mapato la asilimia 9.2.

Juhudi kubwa zilifanywa zilizopelekea kuanzishwa kwa utekelezaji wa kuyaendeleza Maeneo Huru ya Uchumi kwa vitendo. Mradi wa Ujenzi wa Mji Mpya wa Fumba umeanza, ambapo kiwanda kikubwa cha maziwa kimejengwa na kimeanza kazi Julai, 2014. Mji huo utajumuisha ujenzi wa nyumba 650 zitakazouzwa

kwa watu mbali mbali. Ujenzi wa nyumba hizo unatarajiwa kuanza Februari mwaka huu.

Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mradi wa ujenzi wa mji wa kisasa wa kibiashara pamoja na hoteli kubwa za kisasa, nyumba za kuishi, uwanja wa ndege mdogo na uwanja wa kimataifa wa "golf " wa kisasa vitajengwa. Kampuni ya "Pennyroyal ya Gibralter" imetenga jumla ya Dola za Kimarekani milioni 800 kwa ajili ya mradi huu. Kampuni hiyo hivi sasa inaendelea na ujenzi barabara ya kisasa inayotoka Mkwajuni kupitia Kijini hadi Mbuyutende na imefikia hatua nzuri.

Katika kuliendeleza eneo la Bwawani, mnamo mwezi wa Novemba 2015, Serikali ilitiliana saini Mkataba na Kampuni ya "Quality Group Limited" ambayo itaanzisha mradi mkubwa wa kuendeleza Hoteli ya Bwawani na maeneo yaliyoizunguka. Kampuni hiyo imetenga Dola za Marekani zipatazo Milioni 200 kwa ajili ya mradi huo. Kadhalika, kampuni hiyo itajenga majengo ya biashara na kituo cha mikutano ya Kimataifa katika eneo hilo la Bwawani.

Aidha, Serikali imeidhinisha mradi wa uimarishaji wa Hoteli ya "Mtoni Marine", wenye lengo la kutengeneza ufukwe maalum kwa ajili ya mapumziko ya wageni na wenyeji. Sambamba na uimarishaji huo, utaanzishwa mji mdogo wa kisiwa kwa lengo la kuikuza sekta ya utalii.

Katika mwaka wa fedha, 2015/2016, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) imeanza kutekeleza Mradi wa ujenzi wa nyumba za kisasa katika eneo la Mbweni – Unguja. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa jumla ya majengo 18 ya ghorofa 7 kila moja na yatakapomalizika, jumla ya nyumba (flats) 252 zitapatikana. Mradi huu unatarajiwa kumalizika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Kama ilivyokuwa katika miaka mingine ya nyuma, mwaka 2015, suala la kuimarisha mazingira ya biashara lilipewa umuhimu mkubwa. Serikali ilichukua hatua ya kuhakikisha kuwa bidhaa za chakula zinakuwepo nchini wakati wote. Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2015 hakukuwa na upungufu wa bidhaa hizo.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililinunua jumla ya tani 2,826.5 za karafuu 2,826.5 zenye thamani ya TZS bilioni 39.5 kutoka kwa wakulima katika mwaka 2014/2015, hadi kufikia tarehe 4 Januari, 2016, Serikali ilinunua jumla ya tani 3,235.1 zenye thamani ya TZS bilioni 45.3.

Kwa upande wa mauzo, katika mwaka 2014/2015, Serikali iliuza nchi za nje jumla ya tani 2,766.2 za karafuu zenye thamani ya TZS bilioni 53.3. Kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2015, Serikali imeuza karafuu nchi za nje tani 2,122.0 zenye thamani ya TZS bilioni 36.0. Msimu wa karafuu wa mwaka huu bado unaendelea na wakulima wanaendelea kuuza karafuu zao ZSTC na matarajio ya Serikali ni kununua tani 5,500 za karafuu.

Kadhalika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya TZS milioni 342.3 kwa wakulima 126 wa karafuu wa Unguja na Pemba. Mikopo hiyo imewasaidia kununua pembejeo na vitendea kazi.

Aidha, kwa lengo la kuliendeleza zao la karafuu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilizindua Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu Zanzibar ambao Shirika la ZSTC limeweza kulipa fidia kwa walioanguka kwenye mikarafuu jumla ya TZS milioni 60 na kutoa mikopo.

Juhudi za kufufua viwanda nazo zilipata mafanikio makubwa katika mwaka 2015 ikilinganishwa na miaka iliyopita. Bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa mwaka 2015 zikiwemo maziwa, sukari, maji ya kunywa, unga wa ngano, juisi, sabuni, bidhaa za nguo na viungo zilikuwa na thamani ya TZS bilioni 136.0, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.51 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo bidhaa zilizozalishwa nchini zilikuwa na thamani ya TZS bilioni 128.9.

Idadi ya watalii wanaoitembelea Zanzibar imeendelea kuongezeka kutokana na vivutio viliopo, pamoja na kuwepo amani na utulivu. Jumla ya watalii 254,699 waliitembelea Zanzibar katika kipindi cha Januari-Novemba, 2015.

Kwa upande wa kilimo, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya asilimia 75 kwa wakulima ya gharama za pembejeo za kilimo na huduma za matrekta kwa Unguja na Pemba. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016, tayari tani 750 za mbolea na lita 15,000 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa kwa lengo kuwapa wakulima ili kuimarisha kilimo.

Kwa upande wa uendelezaji wa maliasili, Serikali inaendelea



kusimamia ulinzi na udhibiti wa misitu ikiwemo msitu wa Jozani Unguja, msitu wa Ngezi Pemba na misitu mingine ya asili kwa kushirikiana na wananchi. Juhudi zitaendelea kufanywa kuwahamasisha wananchi juu ya ufugaji nyuki wa kisasa biashara ambayo imeonekana kuwa na tija kubwa hasa kwa akina mama na haiathiri mazingira.

Jitihada kubwa zilifanywa katika kuiendeleza sekta ya uvuvi. Katika mwaka 2015, kiwango cha samaki waliovuliwa kilifikia tani 31,439.0 zenye thamani ya TZS bilioni 123.80 ikilinganishwa na tani 30,108.6 zenye thamani ya TZS bilioni 116.3 zilizovuliwa mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 6. Uzalishaji wa zao la mwani pia umeongezeka kutoka tani 13,301 mwaka 2014 hadi kufikia tani 15,076 mwaka 2015. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 13.

Hivi karibuni Serikali inatarajia kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki huko Beit el Ras kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA). Kadhalika, Serikali imetiliana saini makubaliano ya awali na Kampuni ya Hairu kutoka Sri-Lanka ambayo itawekeza katika kiwanda cha kutengeneza boti zenye urefu wa mita 6, na mita 9 kwa ajili ya wavuvi wadogo na mita 18 zitakazofika bahari kuu.

Juhudi mbali mbali zimechukuliwa katika kuimarisha sekta ya ufugaji na hivyo kuongeza hamasa katika ufugaji wa kisasa na kuongeza idadi ya wafugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa kutoka wafugaji 9,795 mwaka 2014 hadi kufikia 10,082 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 2.9.

Kwa lengo la kukabiliana na uharibifu wa mazingira, jitihada zinaendelea kuchukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kukabiliana na athari za kimazingira pamoja na kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira vinavyosababishwa na shughuli za ujenzi, ukataji wa miti ovyo, utupaji wa taka za plastiki ngumu na vifaa vya kielektroniki.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli na viongozi mbali mbali wakifuatilia gwaride la majeshi ya ulinzi na usalama katika kilele cha sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan Studium Mjini Unguja tarehe 12 Januari, 2016,

Kuhusu miundombinu, katika mwaka 2015 Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara za lami mbili ambazo ni barabara ya Konde hadi Wete (km.15) na kutoka Wete hadi Konde (km.15). Ujenzi wa barabara za lami sasa unaendelea katika barabara ya Ole hadi Kengeja huko Pemba (km. 35). Kwa barabara za Unguja ujenzi unaendelea kwa barabara za Jendele kupitia Cheju hadi Kaebona (km. 11.7) na Koani hadi Jumbi (km. 6.3) na Mwanakwerekwe hadi Fuoni (km. 4). Kadhalika, Serikali inaendelea kuifanyia matengenezo makubwa ya barabara ya Ole hadi Konde kuanzia eneo la Meli 5 hadi Chwale (km. 13) huko Pemba kwa kufumuliwa na kutiwa lami upya.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali kwa upande wa Unguja ina lengo la kujenga barabara ya Bububu kupitia Mahonda hadi Mkokotoni (km30), barabara ya Matemwe-Mbuyutende-Muyuni (km 11.5), Pale hadi Kiongele (km 5), Mkwajuni-Kijini-Mbuyutende (km 9), barabara kutoka Fuoni hadi Kombeni (km 7). Kwa upande wa Pemba itajengwa upya barabara ya Wete hadi Chake Chake (km 22.1). Wito wangu kwa wananchi ni kuendelea kuzitunza barabara zetu na kutoa ushirikiano kwa Serikali na wakandarasi wanaojenga barabara zetu.

Kadhalika Serikali imekamilisha matayarisho yote ya ujenzi wa bandari ya Mpigaduri katika mwaka 2015. Ujenzi wa bandari hii unategemewa kuanza katika robo ya kwanza ya mwaka 2016. Aidha, katika mwaka 2015, Serikali imejenga gati ndogo katika Kisiwa cha Tumbatu inayotarajiwa kumalizika mwezi Februari, 2016 na imekamilisha matengenezo ya jengo la abiria katika bandari kuu ya Malindi.

Katika azma ya kuimarisha usafiri wa baharini, Serikali ilitengenezesha meli mpya MV Mapinduzi II katika kampuni ya Daewoo ya Jamhuri ya Korea. Meli hio iliwasili nchini tarehe 2 Disemba, 2015. Meli ya MV Mapinduzi II yenye uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na mizigo tani 200, imeanza ratiba zake tarehe 8 Januari, 2016 kwa safari ya kwenda Pemba. Vile vile, Serikali imeamua kununua meli nyengine mpya ya mafuta mwaka huu.



Kwa upande wa usafiri wa anga Serikali imechukua hatua madhubuti za kuimarisha usafiri wa anga kwa kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na kuweka taa za kisasa za kuongozea ndege katika uwanja wa ndege wa Pemba. Kwa hatua hiyo kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar hivi sasa ndege zinaweza kutua na kuruka wakati wa usiku.

Katika kuimarisha huduma za umeme, kuanzia mwezi Januari hadi Novemba, 2015, kazi kubwa ya uwekaji wa laini za umeme imefanywa, ambapo kilomita 47.25 za laini ndogo na kilomita 31.85 za laini kubwa ya umeme zimewekwa Unguja na Pemba. Kazi ya kupeleka umeme katika visiwa vya Makoongwe na Kisiwapanza huko Pemba imekamilika.

Suala la mafuta na gesi asilia nalo Serikali tayari imelifanyia kazi na imekamilisha Rasimu ya Sera ya Mafuta na Gesi. Rasimu ya sheria ya Mafuta na Gesi asilia ipo katika hatua za mwisho za matayarisho na inatarajiwa kukamilika baada ya muda si mrefu.

Jitihada kubwa zimefanywa na Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuimarisha elimu. Idadi ya skuli za maandalizi zimeongezeka na zimefikia 270 katika mwaka 2015, skuli za msingi zimeongezeka kutoka skuli 359 mwaka 2014 hadi skuli 370 mwaka 2015 na skuli za sekondari zimeongezeka na kufikia skuli 263 mwaka 2015 kutoka skuli 210 mwaka 2014. Idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu vitatu vya Zanzibar imefikia



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiteta na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kilele cha sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar,zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan Studium Mjini Unguja, tarehe 12 Januari, 2016

5,923, hadi kufikia mwezi wa Novemba mwaka 2015. Kadhalika idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo katika vyuo vya ndani na nje ya Tanzania sasa imefikia 3,016 ambapo jumla ya TZS bilioni 9.3 zilitengwa mwaka jana kukidhi mikopo hiyo. Hadi sasa wanafunzi 1,016 wameanza kurejesha mikopo yao kati ya wanafunzi 3,800 waliohitimu masomo yao.

Juhudi maalum zimechukuliwa na serikali katika kuiendeleza sekta ya afya ikiwemo kuifanya Hospitali ya Mnazi mmoja kuwa ya Rufaa. Ujenzi wa jengo la utibabu wa watoto na wagonjwa wenye matatizo ya figo unaendelea vizuri ambapo tarehe 5 Januari, 2016 umewekewa jiwe la msingi pamoja na jengo lilokuwa la kiwanda cha madawa kuanza kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa ajili ya huduma za mama wajawazito na watoto. Sambamba na hatua hiyo, kazi za kuzipandisha daraja hospitali ya Koteji ya Makunduchi na Kivunge zinaendelea vizuri.

Aidha, hospitali ya Abdalla Mzee Pemba nayo imeanza kujengwa upya kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Hospitali hii inatarajiwa kuwa ya kisasa yenye uwezo wa kutoa huduma zote za utibabu na uchunguzi wa maradhi na itakuwa na hadhi ya hospitali ya rufaa ya Mkoa.

Kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa dawa, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka TZS bilioni moja kwa mwaka 2013/2014 hadi kufikia TZS bilioni 4.3 kwa mwaka 2015/2016. Gharama za kuchangia huduma za uchunguzi wa maradhi kwa kutumia “X-Ray”, “CT-Scan” na “Ultra Sound”, zimeondolewa hivi sasa zinatolewa bila ya malipo kwa wananchi wote.

Kutokana na jitihada za kuwasomesha madaktari Serikali imepata mafanikio ya kutia moyo katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa uwiano wa daktari kwa wananchi wanaohudumiwa. Kwa sasa uwiano wa daktari na idadi ya watu anaowahudumia ni daktari mmoja kwa watu 8,885 (1:8885), kutoka kiwango cha daktari mmoja kwa watu 9,708 (1:9708) mwaka jana. Kiwango hicho ni kizuri ikilinganishwa na karibu mataifa yote ya Bara la Afrika.

Sekta ya habari nayo imezidi kuimarika. Jitihada zimeendelea kuchukuliwa katika kuimarisha shughuli za Shirika la Utangazaji la Zanzibar pamoja na Gazeti la Zanzibar Leo. Kupitia vyombo vya habari vya Serikali, Serikali imetekeleza vyema wajibu wake wa kuielimisha jamii na kuipa habari na burudani.

Aidha, Serikali imetekeleza ahadi yake iliyoahidi ya kujenga Studio ya kisasa ya muziki na filamu kwa ajili ya wasanii wa Zanzibar katika jengo lilokuwa la Sauti ya Tanzania Zanzibar liliopo Rahaleo. Studio hiyo ilizinduliwa rasmi tarehe 8 Januari, 2016 na itakuwa inatumiwa na wasanii ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Kuhusu sekta ya michezo, Serikali iliadhimisha kwa mafanikio makubwa siku ya mazoezi inayofanyika kila mwaka ifikapo tarehe mosi Januari kwa lengo la kuhamasisha umuhimu wa kufanya mazoezi, kwa madhumuni ya kuzitunza afya za wananchi.

Katika mwaka 2015 Serikali imeendelea kuchukua hatua ya kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa kadri hali ya ukuaji wa uchumi ilivyoruhusu. Katika mwaka huo wa 2015, Serikali ilifanya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wenye uzoefu na elimu ya kiwango cha Stashahada ambao utumishi wao umefikia zaidi ya miaka 15. Zoezi la kuwapanga watumishi wote wa

Serikali kulingana na madaraja yao limekwishaanza kwa hatua za awali za kukusanya taarifa, ili kazi hiyo ifanywe kwa uangalifu mkubwa na kupata ufanisi.

Kadhalika Serikali imeendelea kuchukua hatua ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kupambana na umaskini. Kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, hadi kufikia mwezi Novemba 2015, jumla ya mikopo 286 yenye thamani ya TZS milioni 436.2 imetolewa. Mikopo hiyo imewanufaisha wananchi wapatao 8,976. Kuanzia Januari hadi Novemba, 2015, jumla ya TZS milioni 397.2 zilikusanywa ikiwa ni marejesho ya mikopo hio. Aidha, Serikali ilisajili taasisi 4 za Wakala binafsi za ajira na kuongeza idadi ya taasisi hizo kufikia 8. Jumla ya vijana 240 wamepata ajira kupitia mawakala hao wa ajira.

Kwa lengo la kuwasaidia vijana kuondokana na tatizo la ajira, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeongeza fedha za dhamana katika Benki ya CRDB kutoka TZS milioni 100 hadi TZS milioni 150 katika mwaka 2015. Kutokana na hatua hiyo, Benki ya CRDB imeweza kutoa mikopo yenye thamani ya TZS milioni 975.3 kwa vijana 2,952.

Aidha, kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha wazee, kuanzia mwezi Aprili mwaka 2016, Serikali itaanza utaratibu wa kuwalipa wazee waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea kiasi cha TZS 20,000 kwa mwezi. Zoezi la usajili linaendelea ambapo tayari jumla ya wazee 22,443 waliostaafu Serikalini na waliokuwa hawajafanya kazi Serikalini wamekwishasajiliwa. Utaratibu huo hauathiri ule wa zamani na wale waliostaafu Serikalini wataendelea kupata pensheni yao ya kisheria. Hatua hiyo inakwenda sambamba na malengo ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964 katika kuwatunza wazee kwa kuwapatia huduma za makaazi na huduma zote nyengine muhimu za kijamii.



Kuhusu watu wenye ulemavu, Serikali imechukua hatua za kuhakikisha kuwa wanapatiwa haki zao na kuwekewa mazingira mazuri yanayozingatia mahitaji yao pamoja na kushirikishwa katika masuala mbali mbali ya kijamii na kitaifa. Kadhalika, jitihada zimefanywa na Serikali katika kuwashirikisha kinamama katika masuala ya maendeleo pamoja na kulinda haki zao kwa kupiga vita vitendo vyote vya udhalilishaji wanawake na watoto ambapo Serikali ilianzisha kampeni hiyo mwaka jana. Kampeni hii inaendelea vizuri ingawa bado kuna changamoto.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbali mbali kama inavyoonekana katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita wa 2015, Serikali ilikabiliwa na changamoto kadhaa, katika utekelezaji wa mipango yake.

Baadhi ya changamoto hizo zimeanza kushughulikiwa na nyengine zinaendelea kufanyiwa kazi.

Itakumbukwa kwamba, Zanzibar iliingia katika Uchaguzi Mkuu tarehe 25 Oktoba, 2015 ambapo wananchi wa pande zote mbili za Muungano walipata fursa ya kuwachagua Viongozi wao.

Uchaguzi wa Viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliosimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umemalizika na Chama cha Mapinduzi kimepata ushindi mkubwa.

Kwa upande wa Zanzibar, Tume ya Uchaguzi iliufuta uchaguzi wa Zanzibar tarehe 28 Oktoba, 2015, baada ya kubainika kutokea kwa kasoro kadhaa kama zilivyoelezwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Kadhalika, uamuzi huo wa Tume ulitangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali la tarehe 6 Novemba, 2015 kwamba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeyafuta matokeo yote ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa tarehe 25 Oktoba, 2015 na kwamba uamuzi wa Tume wa tarehe nyengine ya kurudiwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar utatangazwa baadae.

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1984 na Sheria ya Uchaguzi



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiteta na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kilele cha sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar,zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan Studium Mjini Unguja, tarehe 12 Januari, 2016

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa Mwenyekiti. Taarifa ya pamoja ya mazungumzo hayo itatolewa na wajumbe wanaofanya mazungumzo mara tu mazungumzo hayo yatakapokamilika.

Kudumishwa kwa Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yametimiza miaka 52, lazima kwende sambamba na kudumishwa na kuendelezwa kwa Muungano wa Tanzania ambao ifikapo tarehe 26 Aprili mwaka 2016, utatimiza miaka 52 tangu kuasisiwa kwake. Muungano wa Tanzania ni kielelezo muhimu cha umoja wa Watanzania na udugu wa damu uliopo tangu kale na dahari kwa wananchi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi chote tangu kuasisiwa kwake tarehe 26 Aprili, 1964, wananchi wameendelea kunufaika kiuchumi, kisiasa na kijamii pamoja na kujitokeza changamoto ambazo zimekuwa zikifanyiwa kazi kwa ufanisi mkubwa na Kamati ya pamoja katika Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Nne.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana yanatokana na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini.

Namba 11 ya mwaka 1984, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ndio yenye jukumu la kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani. Kutokana na msingi huo, Rais wa Zanzibar amewaomba wananchi waendelee kuishi kwa amani na kupendana huku wakisubiri Tume ya Uchaguzi Zanzibar itangaze tarehe nyengine ya kurudia uchaguzi.

Aidha, katika suala zima la hali ya kisiasa ya Zanzibar, iliyojitokeza baada ya kufutwa kwa Uchaguzi Mkuu, viongozi walishauriana wakutane ili wafanye mazungumzo ya kutafuta suluhu kwa njia ya amani, ili Zanzibar iendelee kuwa na amani, umoja na mshikamano. Hatimaye viongozi hao walikubaliana waanze mazungumzo hayo.

Mazungumzo hayo yanawahusisha viongozi sita, waliopo madarakani na waliostaafu Rais wa Zanzibar na



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipowasili katika kilele cha sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar,zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan Studium Mjini Unguja, tarehe 12 Januari, 2016

# Muziki wa taarab kielelezo cha Zanzibar


Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi kwenye onyesho la taarab lililoandaliwa rasmi na kikundi cha Taifa cha Taarab cha Zanzibar. Onyesho hili lilikuwa maalum kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofikia kilele chake tarehe 12 Januari 2016 katika uwanja wa Amaan mjini Unguja kwa maandamano, gwaride na hotuba.

Muziki wa Taarab una historia ndefu katika sanaa ya muziki nchini Tanzania. Wapenzi wa muziki wa taarab wa zamani waliiweka taarab katika vyanzo kama Taarab ya Tanga, Taarab ya Dar es Salaam, Taarab ya Zanzibar na Taarab ya Mombasa. Wengine wameubatiza jina muziki wa taarab kuwa ni muziki wa mwambao kutokana na kupendwa sana na watu wa mwambao wa pwani.

Historia inatueleza kuwa Sultan Sayyid Barghash wa Zanzibar aliyetawala kati ya mwaka 1870 na 1888, alipeleka wanamuziki wake wawili kwenda Misri kupata taaluma ya upigaji wa Taarab , na waliporudi ndipo mwaka 1905 wakaanzisha klab ya Ikwaan Safaa, kundi ambalo pamoja na kupitia misukosuko mingi bado lipo mpaka leo.

Muziki wa taarab katika siku za hivi karibuni umekuwa ukizidi kujipatia umaarufu siyo tu kwa kutoa burudani kwa wananchi na viongozi wakuu wa kitaifa Zanzibar, lakini umekuwa kielelezo cha Zanzibar katika biashara ya utalii kuwa ndio kivutio cha burudani kwenye hoteli za kitalii.

Aidha, taarab ya Zanzibar imekuwa kivutio cha aina yake kwenye maonesho mbali mbali ya kimataifa ya utalii nchi za nje. Wasanii maarufu wa Zanzibar kama vile marehemu Fatuma Binti Baraka (Bi. Kidude) walijijengea umaarufu mkubwa kujitangaza wao na Zanzibar kwa jumla kutokana na muziki wa taarab.












Matukio mbali mbali yakimuonesha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano Mama Samia Suluhu Hassan na baadhi ya viongozi mbali mbali wakiwa katika taarab rasmi iliyoandaliwa na Kikundi cha Taifa iliyotumbuizwa siku ya tarehe 12 Januari, 2016 usiku katika Ukumbi wa Salama uliopo Hoteli ya Bwawani ikiwa ni kukamilisha shamra shamra za sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar






# Matukio katika Picha

Matukio mbali mbali yaliyofanyika katika kilele cha sherehe za kuadhimisha miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar likiwemo lile la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed shein kuzungumza na wananchi. Sherehe za Mapinduzi hufanyika kila ifikapo tarehe 12 Januari ya kila mwaka
















# Uwekaji wa Mawe ya Msingi wodi ya watoto pamoja na Kinamama Mnazi Mmoja

- Mwelekeo wa kufikia hospitali ya rufaa unazidi kuonekana wazi



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa nasaha zake kwa wananchi pamoja na wafanyakazi wa Hospitali ya mnazi mmoja katika sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi Wodi ya Watoto na upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwa ni katika shamra shamra miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 05 Januari, 2016. Kulia ni Naibu Waziri wa Afya Mahmoud Thabit Kombo na Balozi wa Uholanzi Nchini Tanzania Bw. Jaap Frederiks

Katika kuadhimisha miaka 52 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliweka mawe ya msingi ya majengo mawili muhimu katika hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Miradi ya majengo hayo yanazidi kuiongezea uwezo hospitali hiyo na kuweza kupanua huduma zake kwa upeo na ufanisi zaidi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa serikali wa kuipandisha daraja hospotli hiyo kuwa ya rufaa.

Majengo hayo ni jengo la wazazi na watoto wachanga ambalo awali lilikuwa kiwanda cha dawa miaka ya 60 na 70. Jengo hilo linafanyiwa ukarabati mkubwa na kuongezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Ufalme ya Uholanzi kupitia shirika ORIO.

Chini ya makubaliano hayo gharama za mradi huo ambao ni Euro milioni 9.9 zitatolewa sawa kwa sawa na kila upande. Mradi huo unatarajiwa kukamilika Julai 2017 ambapo jengo litakaa chini ya uangalizi wa mkandarasi hadi mwaka 2021.

Jengo hilo litakapomalizika litakuwa na vitanda 100, vyumba vya kifafa cha mimba, vyumba vya watoto 40 waliozaliwa, vyumba 8 vya uangalizi, 6 vya unyonyeshaji, vyumba 5 vya kuzalia na vyumba 2 vya upasuaji.

Aidha, sehemu ya chini ya jengo hilo kutakuwa na sehemu za ajali na





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia ikiwa ni ishara ya uwekaji wa jiwe la msingi Wodi ya Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja katika shamra shamra za miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 05 Januari, 2016



dharura, vifaa vyote kwa wagonjwa wa dharura, vifaa vya uchunguzi kama x-rays, "utra sound", mtambo wa kuzalisha gesi ya oksijeni na mtambo wa kuchomea taka.

Jengo la pili lililowekwa jiwe la msingi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein lilikuwa ni jengo la watoto wadogo ambalo litakuwa na zaidi ya vitanda 100. Kati ya vitanda hivyo kutakuwa na vitanda vya watoto wenye maradhi ya kuambukiza na maradhi yasiyoambukiza na vitanda vyengine vya wagonjwa wa matibabu ya figo.

Jengo hilo nalo linajengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Norway na msamaria mwema raia wa Norway bwana Tron Mohn.

Gharama za ujenzi ni dola za kimarekani milioni 1.671 ambapo Serikali ya Norway imetoa dola za kimarekani 600,000.00, Bwana Tron Mohn dola za kimarekani 821,378.00 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar dola za kimarekani 250,000.00

Katika hotuba yake kwenye sherehe hizo za uwekaji mawe ya msingi, Mhsehimiwa Rais alisema katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Saba kasi ya uimarishaji wa sekta ya afya imeongezeka na kuifanya Zanzibar kupiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma za afya.

Alifafanua kuwa azma ya kuzipandisha hadhi hospitali za Mnazi Mmoja Zanzibar na Abdalla Mzee Mkoani Pemba pamoja na hospitali za Koteji Unguja na Pemba kuwa za Wilaya imetekelezwa kwa kiwango kikubwa na wananchi hawana budi kujivunia mafanikio hayo.

Dk. Shein alizishukuru serikali na wananchi wa Norway na Uholazi kwa misaada hiyo na mingine ambayo nchi hizo zimekuwa zikitoa kwa Zanzibar.

Aidha, alimshukuru kwa dhati kabisa bwana Tron Mohn kwa ukarimu wake na hisani yake kwa wananchi wa Zanzibar.



Baadhi ya wanafunzi wa Vyuo mbali mbali vya Afya wakiwa katika sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi Wodi ya Watoto na upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwa ni katika shamra shamra miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 05 Januari, 2016



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia kuashiria uzinduzi wa Skuli ya Msingi Mnarani Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba iliyojengwa kwa nguvu za wananchi na ufadhili ya Shirika la Milele Foundation la Zanzibar ufunguzi huo umefanyika katika shamra shamra za kusherehekea miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 07 Januari, 2016. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Bi. Khadija Bakari na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Muheshimiwa Ali Juma Shamuhuna

# Wanakijiji wa Mnarani Pemba wafurahia kupata skuli ya kisasa

Tukio la ufunguzi wa skuli ya msingi na chekechea katika kijiji cha Mnarani, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kusini Pemba ni tukio la kihistoria ambalo limeleta furaha na faraja kwa wakaazi wa kijiji hicho na vijiji jirani vya Misheshelini na Mawe Matatu.

Uzinduzi wa skuli hiyo uliofaywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ilikuwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo moja ya malengo yake ilikuwa ni kuweka hali za wananchi sawa ikiwemo upatikanaji wa elimu.

Skuli hiyo ya kisasa iliyojengwa kwa ushirikiano kati ya wananchi, serikali na Taasisi isiyokuwa ya serikali ya Milele Zanzibar Foundation, inatoa fursa kwa watoto wa vijiji hivyo ambao kabla ya skuli hiyo walilazimika kutembea masafa marefu kufuata skuli na baadhi yao kuacha masomo njiani, kuanza masomo wakiwa na umri mkubwa au kutokwenda skuli kabisa.

Hatuna budi kupongeza ushirikiano na mshikamano uliooneshwa kati ya wananchi, serikali na Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation hadi kukamilisha ujenzi wa skuli hiyo kwa kiwango cha juu.

Wahenga walisema kuwa “kuzaa mwana si kazi, kazi ni kulea” hivyo tunaunga mkono wito wa Mheshimiwa Rais kwa wananchi kuwataka wazazi na walezi kufuatilia kwa karibu maendeleo ya elimu ya watoto wao maskulini ili hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali kama hii ya kujenga skuli hii kuimarisha elimu ziweze kufikia malengo yaliyowekwa.

Dk. Shein aliwahakikishia wananchi kuwa serikali itaendelea kuimarisha sekta ya elimu ili kutimiza malengo ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ya kuwapatia elimu wananchi wote.

“Tulilazimika kufanya Mapinduzi kukomesha kila aina ya dhulma dhidi ya wananchi wanyonge wa Zanzibar na kazi yetu sasa ni kuhakikisha malengo ya Mapinduzi yanatekelezwa na kila mwananchi anafaidika kwa kuchukua hatua madhubuti za kuwapatia huduma kama hizi” Dk. Shein aliwaeleza wananchi hao katika hotuba yake ya uzinduzi.

Skuli ya Mnarani ina uwezo wa kuchukua watoto 310 lakini kwa mujibu wa taarifa ya skuli hiyo, tayari watoto 477 wameshaandikishwa. Taarifa hiyo inaonesha kuwa kiwango cha uandikishaji watoto kimezidi asilimia 100 kwa mwaka 2016.

Hata hivyo, kwa mujibu wa takwimu za jumla za uandikishaji



wa watoto kwa wilaya nzima ya Micheweni si ya kuridhisha ambapo kwa upande wa elimu ya maandalizi kiwango cha uandikishaji ni asilimia 35.6 tu wakati sekondari ni asilimia 40.3 tu.

Na ndio maana Mheshimiwa Rais alikuwa na ujumbe maalum kwa wazazi na walezi katika wilaya hiyo kwa kuwataka wahakikishe kuwa watoto wote waliotimiza umri wa kwenda skuli wanaandikishwa na wanahudhuria masomo.

Hata hivyo, hakusita kuwapongeza wananchi wa Mnarani katika wilaya hiyo ambapo kiwango cha uandikishaji watoto wenye umri wa kwenda skuli ni zaidi ya asilimia 100.

Pamoja na kuishukuru Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation kwa kuchangia kwa kiwango kikubwa ujenzi wa skuli hiyo ambayo ujenzi wake wote uligharimu shilingi milioni 359.377 Mheshimiwa Rais aliahidi kuipatia skuli hiyo kompyuta moja iliyokamilika pamoja na mashine ya kurudufia (Photopy machine) baada ya kazi ya kuweka umeme kukamilika katika skuli hiyo.

Ni Baadhi ya matukio mengine aliyoyafanya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati wa uzinduzi wa Skuli ya Msingi Mnarani Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba tarehe 07 Januari, 2016.



# Dk. Shein aandika historia mpya Pemba




■ Awa Rais wa mwanzo kuruka usiku uwanja wa ndege wa Pemba



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya viwanja vya Ngege Zanzibar Kepten Saidi Iddi Ndumbugani kuhusu aina ya Taa mbali mbali zilizofungwa kwa uongozaji wa Ndege wakati ikitua katika sherehe ya uzinduzi wa Taa za kuongozea Ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Pemba uliofanyika ikiwa ni katika maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 08 Januari, 2016.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein ambaye anaongoza awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, ameandika historia mpya kwa kuwa Rais wa kwanza kuruka kwenye uwanja wa ndege wa Pemba wakati wa usiku mara baada ya yeye mwenyewe kuzindua taa za kuongozea ndege wakati wa usiku kwenye uwanja huo.

Hatua ya kuruka ndege wakati wa usiku katika uwanja wa ndege wa Pemba ni mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa muda mrefu wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha miundombinu ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege.



Baadhi ya Taa za kuongozea ndege zilizojengwa katika kiwanja cha ndege cha Karume Kisiwani Pemba

Katika kuimarisha viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba, serikali imeshapiga hatua kubwa katika kujenga kiwanja kipya cha kisasa "Terminal II" kwa Unguja, na hivi sasa inatekeleza mpango wa kukiimarisha kiwanja cha ndege cha Pemba kufikia kiwango cha kimataifa.

Moja kati ya hatua za karibuni zilizochukuliwa na Serikali ni kukamilisha uwekaji wa taa za kuongozea ndege ambazo zitakiwezesha kiwanja hicho kutoa huduma za kuruka na kutua ndege wakati wote.

Itakumbukwa kwamba shughuli hiyo ambayo ni miongoni mwa shamrashamra za maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, ni ahadi ya Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein aliyoahidi mwaka 2010 wakati alipokwenda kuomba ridhaa kwa wananchi kutaka kuongoza nchi.

Katika hotuba yake Dk. Shein alisisitiza dhamira ya serikali ya kuhakikisha kuwa kiwanja hicho kinaimarishwa na kufikia kiwango cha kimataifa.

Ni dhahiri kuwa kukamilika kwa awamu hiyo ya mradi ambapo sasa kutawezesha ndege kutua wakati wote katika kiwanja hicho ni kielelezo kingine cha hatua madhubuti zinazochukuliwa na Serikali kutekeleza dhamira yake ya kuimarisha miundombinu ya kiuchumi nchini.

Kwa mujibu wa mpangokazi wa uimarishaji uwanja huo, hatua nyingine inayofuata ni ujenzi wa jengo jipya la abiria na kuongeza urefu wa njia ya kurukia na kutua ndege kutoka kilomita 1.5 za sasa hadi kufikia kilomita 2.5.

Utekelezaji wa hatua hiyo kwa mujibu wa Mheshimiwa Rais unatarajiwa kuanza si muda mrefu kwa vile mazungumzo kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kuhusu kugharimia mradi huo yanaendelea vizuri.

Manufaa makubwa kwa mradi huu ni kuongezeka kwa safari za ndege zikiwemo za kitalii kwa kuweza kuruka na kutua muda wote jambo ambalo litawafanya wageni kuweza kupanga safari zao wakati wowote kwa kadri watakavyopenda.

Kwa hivyo ubora wa huduma za uwanja huu unakwenda sambamba na mpango wa serikali wa kuimarisha biashara ya Utalii nchini kwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar hadi kufikia lengo la watalii 500,000 ifikapo mwaka 2020, ingawa mwenendo wa sasa unaashiria kuzidi kiwango hicho hadi kufikia zaidi ya watalii 700,000, iwapo hali ya amani na utulivu itaendelea kudumu kama ilivyo sasa.

Tunaamini kwamba kuongezeka kwa safari za ndege kisiwani Pemba mbali ya kuongeza ajira kwa wananchi, lakini pia kutaongeza mzunguko wa fedha kutokana na huduma mbali mbali zitakazotolewa kwa wasafiri na wageni na hivyo kuimarisha mapato ya serikali na pato la mtu mmoja mmoja.

Kwa mujibu wa taarifa ya mradi huo, katika awamu hii ya kwanza mafundi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa kushirikiana na wizara ya Miundombinu na Mawasilinao ndio waliosimamia na kutekeleza mradi huo kwa asilimia 98.

Haya ni mafanikio makubwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar hasa ikizingatiwa kuwa Mamlaka hiyo imeundwa miaka minne iliyopita huku ikiwa imekabiliwa na changamoto kadhaa.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Dk. Juma Malik Akil, kazi ya kuweka taa ilifanywa na kampuni ya Safegate kutoka Ujerumani wakati kazi za ujenzi (civil works) zikiwemo za uchimbaji mashimo ya nyaya za umeme na uwekaji wa uzio zimefanywa na kampuni ya SKARS Building Company Ltd ya Zanzibar. Mradi mzima umegharimu shilingi bilioni 1.4



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora Dkt. Mwinyihaji Makame kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia kuashiria kufungua Jengo la Wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A Mkoa wa Kaskazini Unguja, katika shamra shamra za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kutimia miaka 52, tarehe 09 Januari, 2016. Kushoto ni Naibu Waziri wa Afya Mahmoud Thabit Kombo Jecha

# Ufunguzi wa jengo la wagonjwa wa nje Kivunge


Kufunguliwa kwa jengo jipya kwa ajili ya wagonjwa wa nje katika hospitali ya Kivunge, katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa mara nyengine tena kumethibitisha azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya na kuwaondolea wananchi shida zinazohusiana na ukosefu wa huduma za afya.

Ukweli uliowazi kwamba Serikali imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya kuiendeleza sekta ya afya nchini kupitia vitengo na programu mbali mbali zinazoendeshwa na Serikali kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo.

Mafanikio hayo yanaonekana katika hali tofauti ikiwemo kuweko kwa ongezeko kubwa la vituo vya afya vya daraja mbali mbali kiasi kwamba hivi sasa wananchi wa Zanzibar hawawezi kwenda zaidi ya kilomita tano bila ya kukuta kituo cha afya.

Kabla ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, Mkoa wa Kaskazini Unguja ulikuwa na vituo viwili tu vya afya ambavyo vilikuwepo Mkokotoni na Chaani. Miaka 52 baada ya Mapinduzi, Mkoa huo hivi sasa una vituo vya afya 26. Vituo 18 ni vya daraja la kwanza na vituo 7 vya daraja la pili.

Aidha, kuna hospitali ya koteji ya Kivunge ambayo lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba ni kuipandisha daraja kuwa hospitali ya wilaya pamoja na hospitali nyengine zilizoko Makunduchi, Micheweni na Vitongoji. Lengo la





Serikali katika mradi huo ulioanza mwaka 2012, ni kuziimarisha huduma za afya katika hospitali zote za koteji ili hatimaye kupunguza msongomano wa wagonjwa katika hospitali kuu ya Mnazi mmoja.

Kadhalika, Serikali imekusudia kuzisogeza huduma za afya kuwa karibu zaidi na wananchi ikiwa ni pamoja na huduma za upasuaji kwa kinamama wajawazito, huduma za uchunguzi, kama vile za maabara, "X-ray" na "Ultra-sound".

Katika kuyaimarisha mazingira ya kutolea huduma, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, imefanya matengenezo makubwa ya wodi za wagonjwa wanaume, wodi ya kinamana na wodi ya watoto. Kadhalika, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo nyumba 12 za wafanyakazi zimezifanyiwa matengenezo makubwa pamoja na kuzijengea ukuta.

Juhudi hizo za Serikali zinaweza kuleta tija iwapo wananchi wote watakuwa tayari kuzitumia fursa za kuwepo na kuimarika kwa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya katika kupata matibabu. Ni kweli kwamba tiba mbadala zipo lakini ni bora zikiwa zinatolewa na wataalamu wa afya.

Miongoni mwa tiba mbadala zinazosisitizwa hasa kwa maradhi kama presha na sukari ni kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi. Kufanya mazoezi ni tiba na ni kinga kwa maradhi mbali mbali yasiyo ya kuambukiza. Aidha, njia nzuri

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini akimsalimia Mtoto Nazna Ali Silima aliyefika kupima mwenye miezi 5 uzito kilo 7.3 katika Hospitali ya Kivunge wagojwa wa nje, baada ya kifungua Hospitali hiyo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 09 Januari 2016. Jengo hilo limejengwa kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali (HIPZ) kutoka Uingereza. Katikati ni Dkt.Tamim Hamad Said Daktari Dhamana Hospitali ya Kivunge na Muuguzi Filonema Raumond Woga





Wawakilishi wa Mashirika ya Misaada ya kimaendeleo ambayo yamesaidia vifaa mbali mbali wakitoa salamu zao wakati wa ufunguzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A. Unguja lililofunguliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika shamra shamra za miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 09 Januari, 2016

nyengine ya kuepukana na aina hiyo ya maradhi ni kuwa na utamaduni wa kupima afya badala ya mtu kusubiri hadi maradhi hayo yanakuwa sugu kutibika. Wazee walisema "kinga ni bora, kuliko tiba."

Kadhalika, kuna haja ya kuongeza jitihada katika usafi wa mazingira, kutumia vyoo na kuhimizana juu ya haja ya kunawa mikono kabla ya kula na kuhifadhi vyakula na kuchemsha maji ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza hasa kipindupindu. Ugonjwa huu upo katika maeneo mbali mbali nchini. Kwa hivyo, kila mmoja anapaswa kuchukua hatua za kukabiliana nayo na kuutokomeza kabisa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini akipokea Kadi ya Mfuko wa Taifa wa Afya Kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa mfuko huo Bw. Michael Mhando kadi hiyo imetolewa kwa ajili ya Mzee Makame Mjombo wa Gamba mweye umri wa zaidi ya miaka 100, wakati wa sherehe za ufunguzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A. Unguja lililofunguliwa kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, ikiwa ni katika shamra shamra za miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 09 Januari, 2016



# Dk. Shein ametaka studio ya kurekodia muziki, filamu itumike kuinua vipaji

Ufunguzi wa studio ya kurekodia muziki na filamu - Rahaleo ni miongoni mwa hatua za utekelezaji wa ahadi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ambazo alizitoa katika nyakati tofauti mwaka 2010, wakati alipokuwa akiomba ridhaa ya wananchi kuongoza nchi.

Hatua hiyo ilikuja kutokana na kilio cha muda mrefu cha wasanii wa Zanzibar hasa wanamuziki ambao walikosa kabisa studio ya kisasa ya kurikodia kazi zao. Wasanii hao walilazimika kwenda katika studio mbali mbali ambazo baadhi yake hazikuwa na hadhi wala haiba inayolingana na umahiri wa wasanii wenyewe.



"Leo namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa ahadi niliyoiweka kwenu ya kuwajengea studio hii yenye haiba na vifaa vya kisasa ambayo itakuwezesheni kurikodi kazi zenu kwa mujibu wa hadhi na uwezo wenu. Nafahamu kwamba baadhi ya studio mlizokuwa mkitumia hapo kabla zilikutozeni fedha nyingi, jambo ambalo lilizorotesha juhudi zenu; hasa wasanii chipukizi ambao walishindwa kumudu gharama walizolazimika kulipia". Alisema Dk. Shein

Dk. Shein alisema ana imani kuwa Studio hiyo ya kisasa itakuwa ni chemchem ya kukuza vipaji vya wasanii hapa Zanzibar kwa kutambua kwamba hata wasanii chipukizi watapata fursa ya kwenda kufanya kazi zao bila ya kujali ukubwa wa mitaji waliyonayo na idadi ya washabiki wanaopenda kazi zao.

Ingawa ujenzi wa kituo hicho umeigharimu Serikali fedha nyingi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Shein ililazimika kutekeleza mradi huo kutokana na kutambua umuhimu wa sanaa kwa maendeleo ya nchi pamoja na shida zinazowapata wasanii wakati wanapotaka kufanya kazi zao.

Miongoni mwa majukumu ya msingi ambayo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utamaduni na Michezo imekabidhiwa katika kukiendeleza kituo hicho, ni kuhakikisha kuwa studio hiyo inajiendesha wenyewe bila ya kuathiri juhudi za wasanii, kwani lengo la Serikali kwenye kituo hicho ni kuona kwamba sekta hii ya Sanaa kwa upana wake, iwe ya ufundi, uchoraji, uandishi, muziki, maigizo, filamu na nyenginezo, inapata mafanikio na inatoa ajira kwa wasanii wa fani zote na wanaishi maisha bora zaidi.

Sanaa inayo nafasi kubwa ya kuitangaza Zanzibar pamoja na kuimarisha na kukuza mila, utamaduni, na desturi za watu wake. Aidha, sekta hii ya sanaa inachukua umuhimu









Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa na viongozi wengine wakiangalia moja ya filamu iliyooneshwa wakati wa ufunguzi rasmi wa Studio ya Muziki na Filamu katika jengo la zamani la Studio Rahaleo Mjini Unguja, mara baada ya kufanyika ufunguzi huo ikiwa ni shamra shamra za Mapinduzi ya Zanzibar kutimia miaka 52, tarehe 09 Januari, 2016

wa pekee katika kuimarisha umoja na mshikamano wa Wazanzibari, kupanua wigo wa ajira na bila ya shaka inaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha ukuaji wa Pato la Taifa.

Historia inaonesha kwamba mataifa yote yenye nguvu kubwa za kiuchumi na kisiasa duniani hivi sasa, yalitumia sekta ya sanaa kama ni nyenzo muhimu ya kujenga himaya zao ndani ya nchi, na kwa kiasi kikubwa, nje ya mipaka yao. Mataifa haya hadi sasa yanaendelea kutumia sekta ya sanaa katika kueneza proganda, ajenda na kutangaza pamoja na kuendeleza mipango yao ya kiuchumi na kijamii.

Siyo vibaya na kwa kweli itapendeza sana iwapo Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo kwa kushirikiana na wasanii wazalendo wakadhamiria kuifanya sekta hiyo nchini kuwa kama au zaidi ya mataifa yaliyoendelea.

